



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. P.40/HMM/VOL.XII/62

Tarehe: 27 Agosti, 2021

TANGAZO

NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wananchi wenye sifa zinazotakiwa ili kujaza nafasi ifuatayo:-

1. Katibu Muhtasi Daraja III – Nafasi 1

1.1 Sifa za Mwombaji

Awe amehitimu kidato cha IV na kuhudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Window, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

1.2 Majukumu ya Kazi

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majadala, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

Masharti ya jumla

- Waombaji wote wawe na umri usiozidi mika **45**
- Barua ya maombi ya kazi **iliyosainiwa** iambatishwe na:-
 - Maelezo binafsi (CV)
 - Nakala za vyeti vya kuhitimu (kidato cha nne au sita, cheti cha kuzaliwa na vyeti vya mafunzo (taaluma)
 - Picha ndogo mbili za "Passport".

NB: Maombi yasiyozingatia masharti haya hayatashughulikiwa.

Namna ya kutuma maombi.

Maombi yatumwe kwa:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA,
S.L.P. 194,
MUSOMA**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14 Septemba, 2021

Limetolewa na:-



Bosco O. Ndunguru

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**